# OPENER STD 5 TERM 2 2020
# KISWAHILI ACTIVITIES

NAME……………………………………………………………………………………

Learner's Number [ | | ]

Gender Boy [ ] Girl [ ]

County name ………………………………………… County code [ | | ]

Sub county name ………………………………………… Sub county code [ | | ]

School name ………………………………………… School code [ | | ]

The grid below is to be filled by the teacher after marking the learner's work

| | Level 1 | Level 2 | Level 3 | Level 4 |
|---|---|---|---|---|
| Numbers 1-15 | | | | |
| Measurement 16-23 | | | | |
| Geometry 24-25 | | | | |

*Soma kifungu kifuatacho. kina nafasi* **1 - 15.** *Katika kila nafasi, umepewa majibu manne. Chagua jibu mwafaka kujaza pengo kati ya yale umepewa.*

Mlango __1__ mwalimu __2__ Kiswahili __3__ alikuwa wa __4__ kuingia katika darasa __5__ la tano. Kipindi __6__ asubuhi kilikuwa __7__. Alitusabahi kama __8__ desturi __9__. Baada ya shughuli ndogo ndogo za hapa na pale __10__ darasani, alianza kutuelezea __11__ kuandika hati safi __12__ darasani, __13__ pia maishani __14__. Kisha alituita __15__ ubaoni tukaandika neno hati.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. ulipofungwa | B. ulifunguliwa | C. ulipofunguliwa | D. ulipofungulia |
| **2.** | A. cha | B. kwa | C. wa | D. ya |
| **3.** | A. ndiye | B. ndivyo | C. ndiyo | D. ndio |
| **4.** | A. kuanza | B. kwanza | C. kuanzia | D. kwenda |
| **5.** | A. yetu | B. mwetu | C. kwetu | D. letu |
| **6.** | A. ile ya | B. hicho ya | C. kile cha | D. hii ya |
| **7.** | A. lake | B. chake | C. wake | D. kile cha |
| **8.** | A. ilivyokuwa | B. lilivyokuwa | C. ilikuwa | D. iliyokuwa |
| **9.** | A. mwake | B. yake | C. yetu | D. wetu |
| **10.** | A. mle | B. ule | C. lile | D. zile |
| **11.** | A. jinsi ya | B. vile ya | C. ukweli wa | D. vile ya |
| **12.** | A. sivyo tu | B. siko tu | C. siyo tu | D. sio tu |
| **13.** | A. mbali | B. pale | C. bali | D. vile |
| **14.** | A. yetu | B. mwetu | C. zetu | D. wetu |
| **15.** | A. moja | B. mmoja | C. mmoja mmoja | D. moja moja |

*Kutoka swali* **16** *mpaka* **30** *chagua jibu kulingana na maagizo.*

**16.** Chagua nomino ambayo hupatikana katika ngeli ya U - U.
A. Mwembe  B. Ukuta
C. Jiwe  D. Uwezo

**17.** Kamilisha tanakali:
Sare ya mwanafunzi iliraruka ______!
A. ruu  B. lwa
C. rwa  D. kacha

**18.** Jaza pengo kwa kutumia kivumishi cha idadi.
Adinasi ________ walinusurika kifo.
A. tano  B. wasaba
C. tisa  D. wambili

**19.** Ni ipi si aina ya mavazi?
A. Bulibuli
B. Shubaka
C. Tarbushi
D. Surupwenye

**20.** Tumia '-enye' kujaza pengo.
Mzigo ________ uzito ni huu.
A. mwenye  B. mwenyewe
C. wenye  D. yenye


**21.** Kamilisha tashbihi ifuatayo:
Nzito kama ________.
A. njiwa  B. duma
C. korongo  D. nanga

**22.** Chagua sentensi iliyo na kivumishi cha sifa.
A. Mwanafunzi mwenyewe aliadhibiwa.
B. Kiti hicho ni cha mwalimu.
C. Uteo huo una nafaka.
D. Mti mrefu utakatwa na mkulima.

**23.** Chagua maelezo ya majina ya ukoo yaliyo sahihi.
A. Shangazi ni ndugu wa kiume wa mama.
B. Ami ni ndugu wa kike wa baba.
C. Bavyaa ni mama aliyemzaa mke wako au mume wako.
D. Mulamu ni jina wanaloitana ndugu na mumeo.

**24.** Kanusha
Mgeni alifika salama.
A. Mgeni hajafika salama.
B. Mgeni hafiki salama.
C. Mgeni hakufika salama.
D. Mgeni hangefika salama.

**25.** Chagua jina la umbo hili



A. duara dufu
B. mche
C. duara
D. pia

**26.** Andika akisami hii kwa maneno. $\frac{1}{3}$
A. Thuluthi  B. Robo
C. Sudusi  D. Thuluthi tatu

**27.** Jaza pengo kwa kutumia kiashiria cha nafsi mbali zaidi.
Shambani ______ kuna siafu wengi.
A. huku  B. humu
C. kule  D. hapa

**28.** Tumia kiunganishi kifaacho
Mwalimu kinyua alituacha ______ tufanye zoezi.
A. na  B. ili
C. kwa sababu  D. kwa maana

**29.** Andika kwa tarakimu.
Elfu mbili mia mbili na mbili
A. 2022  B. 20202
C. 2222  D. 2202

**30.** Chagua kihusishi katika sentensi hii
"Malaika ameketi juu ya meza ya mama."
A. malaika  B. juu ya
C. meza ya  D. ameketi

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu swali la* 31 – 40**

Watu walikuwa wamezoea kuwabebesha punda mizigo mingi. Kila walipotaka kwenda mahali walimuiita na kumwekelea mizigo yao juu ya mgongo wa punda. Alizoea kubeba mizigo mizito na hakulalamika.

Siku moja watu walimwita punda aliyekuwa na mtoto mdogo na kumwambia "leo mizigo imekuwa mingi sana, mwanao atakusaidia kuibeba." Punda alikasirika na kusema kwamba ataibeba peke yake. "Tafadhali msibebeshe mwanangu mizigo."

Watu hao hawakumsikia punda. Walimbebesha mizigo na pamoja na mwanawe pia. Walipoliwa njiani punda alimwangalia mwanawe na kuona amechoka sana, kwa hasira nyingi, punda huyo alijitupa chini na kukataa kuendelea na safari.

Alipigwa sana lakini alikataa katakata kuendelea na safari.

Mwishowe watu waliondoa mizigo na kuiweka chini. Alipoona mwanaye amepumzishwa alisimama na kuanza. Watu wao walielewa kuwa, uchungu wa mwana aujuaye mzazi.

**31.** Punda alikuwa
A. habebi mizigo mingi.
B. akibeba mizigo michache.
C. akibeba mizigo mingi
D. hapendi kubeba mizigo mingi.

**32.** Punda hakulalamika kwa sababu ya
A. ujinga wake
B. tabia ya kupenda watu.
C. kupewa chakula kingi
D. mazoea

**33.** Mizigo iliwekelewa
A. mgongoni mwa punda.
B. katika tumbo la punda.
C. miguuni mwa punda.
D. kichwani mwa punda

**34.** Mtoto wa punda huitwaje
A. kitungule
B. kihongwe
C. chotara
D. shibli

**35.** Punda alikasirika
A. aliponyimwa chakula
B. mwanawe aliponyimwa chakula.
C. mwanawe alipokatazwa kubeba mizigo.
D. mwanawe alipobebeshwa mizigo.

**36.** Mtoto wa punda alitakikana amsaidie mamake kwa sababu
A. jua lilikuwa kali.
B. mizigo ilikuwa mingi.
C. alikubali kumsaidia mamake.
D. mamaye alikataa kubeba mizigo

**37.** Aliyechoka kwanza alikuwa
A. punda na mwanao
B. watu
C. kihongwe
D. punda

**38.** Safari ilipoanza punda waliokuwa wamebeba mizigo walikuwa?
A. watatu B. wanne
C. mmoja D. wawili

**39.** Punda alijitupa chini kwa sababu
A. alikuwa na njaa
B. alichoka
C. mwanawe alilia
D. alimwonea mwanawe huruma.

**40.** Watu walijaribu kumfanya nini ili punda aendelee na safari?
A. Kumbebesha punda
B. Kumpiga punda
C. Kumpa chakula
D. Kumpiga mwanawe

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 – 50***

Ni sharti tuyatunze mazingira yetu. Kinyume cha kutoyatunza mazingira yetu ni kujisababishia maafa na maradhi yasiyokuwa na mwisho. Maradhi kama vile homa ya matumbo husababishwa na mazingira chafu. Aidha, kipindupindu vile vile husababishwa na hali hiyo.

Binadamu huyachafua mazingira yake kwa njia mbalimbali, matumbo ya maji chafu kutoka viwandani huelekezwa kwenye mito. Maji haya machafu huchafua maji safi katika mito. Watu wanapokunywa maji haya machafu, huambukiza maradhi mbalimbali. Baadhi ya watu pia hutupa maganda ya matunda ovyo ovyo, badala ya kuyatupa katika jaa la takataka. Aidha, moshi kutokana na magari huchafua hewa. Watu wanapoivuta hewa hii chafu hupatwa na maradhi yanayohusiana na upumuaji. Ni vyema **tuyatunze** mazingira yetu kwa kupanda miti. Kulinda vianzo vya maji na kudumisha hewa safi.

**41.** Tusipotunza mazingira yetu
- A. tutakuwa wenye afya.
- B. tutaepuka magonjwa.
- C. tutaishi kwa raha.
- D. tutapatwa na maafa.

**42.** Ni maradhi yapi husababishwa na mazingira chafu?
- A. Kiharusi na malaria..
- B. Kikohozi na ukimwi.
- C. Malaria na kifafa.
- D. Kipindupindu na homa ya matumbo.

**43.** Mito huchafuliwa na
- A. wanyama wanaoishi majini.
- B. vitendo vya uvuvi.
- C. maji chafu kutoka viwandani.
- D. moshi itokanayo na magari.

**44.** Kulingana na taarifa, maganda ya matunda
- A. hayapaswi kutupwa katika jaa.
- B. hurembesha mazingira.
- C. huchafua mazingira.
- D. huzuia maradhi.

**45.** Ni jambo lipi kati ya haya huchafua hewa?
- A. Kuelekeza mabomba ya maji chafu mitoni.
- B. Upandaji wa mti.
- C. Kutupa maganda ovyo ovyo.
- D. Moshi kutokana na magari

**46.** Maradhi yanayohusiana na upumuaji hutokana na
- A. hewa chafu.
- B. maji chafu.
- C. magari mengi.
- D. watu wengi.

**47.** Neno **tuyatunze** katika taarifa lina maanisha
- A. tuyachafue
- B. tuyalinde
- C. tuyaharibu
- D. tuyadharau

**48.** Binadamu huchafua mazingira yake kwa kufanya mambo yafuatayo ila
- A. kupanda aina mbalimbali ya miti.
- B. kuelekeza mabomba ya maji chafu mitoni.
- C. kuendesha magari yanayotoa hewa chafu.
- D. kutupa maganda ya matunda ovyo ovyo.

**49.** Mwandishi anasema kuwa tukiyatunza mazingira yetu
- A. tutakuwa wagonjwa.
- B. tutaishi kwa kuzuni
- C. tutaepuka maradhi.
- D. tutapatwa na maafa

**50.** Kichwa mwafaka cha taarifa hii ni
- A. Umuhimu wa kutunza maji
- B. Umuhimu wa maji
- C. Aina ya maradhi
- D. Umuhimu wa kutunza mazingira